JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA
Tovuti: www.hlpc.go.tz
Simu: 0734005777 Barua Pepe:hlpc@afya


# TANGAZO

## KUFUNGUA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI OKTOBA 2024

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inawataarifu wahitimu wote wa Shahada ya kwanza ya Maabara ya Afya ya Binadamu kuwa dirisha la maombi ya utarajali litafunguliwa tarehe **14.10.2024** Saa **4:00 Asubuhi** na kufungwa **15.10.2024 Saa 9:30 Alasiri.** Aidha, Maombi yatafanyika kupitia mfumo wa ***hprs.moh.go.tz***

**Mambo muhimu ya kuzingatia;**

1. Wahitimu wanaoruhusiwa kufanya maombi ya utarajali ni wale walioomba usajili wa awali baada ya kupata barua ya utambulisho kutoka chuoni
2. Wahitimu wote waliosoma nje wanatakiwa kuhakikisha wameambatanisha cheti cha uthibitisho kutoka TCU pamoja na cheti cha matokeo au cheti cha taaluma kutoka chuoni
3. Waombaji wote wanatakiwa wawe wamefanya maombi ya usajili wa awali (Provisional Registration) na awe amepata ujumbe (notification) angalau **yamethibitishwa** (***APPROVED).***
4. Waombaji wote wanasistizwa kufanya maombi kwa wakati na ikitokea mwombaji atahitaji kubadili kituo cha utarajali, anaweza kufanya hivyo kuhamia kituo kingine chenye nafasi kupitia akaunti ya mwombaji ya mfumo wa hprs.moh.go.tz kabla dirisha halijafungwa. Baada ya dirisha kufungwa **HAKUTAKUWEPO NA UWEZEKANO** wa kubadili kituo cha utarajali.

Aidha; Wale wote wataopangiwa vituo vya utarajali wanatakiwa kufika Dodoma Ofisi ya Msajili, Baraza la Wataalam wa Maabara tarehe 26.10.2024 Saa 2:00 asubuhi ili kupatiwa maelekezo pamoja na kupatiwa barua.

Ofisi ya Msajili inawatakia waombaji wote utekelezaji mwema

Imetolewa na

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
07.10.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
07 OCT 2024
P.O. Box 743
DODOMA